

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA SITA

09 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA SITA – TAREHE 09 APRILI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Taarifa za Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 06 la tarehe 05 Februari, 2021;
2. Toleo Na. 07 la tarehe 12 Februari, 2021;
3. Toleo Na. 08 la tarehe 19 Februari, 2021;
4. Toleo Na. 09 la tarehe 26 Februari, 2021;
5. Toleo Na. 10 la tarehe 05 Machi, 2021;
6. Toleo Na. 11 la tarehe 12 Machi, 2021;
7. Toleo Na. 12 la tarehe 19 Machi, 2021; na
8. Toleo Na. 13 la tarehe 26 Machi, 2021.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

38. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inachukua hatua gani kumaliza tatizo la upungufu wa Walimu nchini hasa katika shule zilizopo maeneo ya Vijijini.

39. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mfumo wa ukusanyaji mapato wa GoTHOMIS kwenye Zahanati kama ilivyo kwenye Vituo vya Afya ili kuondoa mwanja wa upotevu wa mapato.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

40. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaendelea kuhuisha miundo ya Utumishi kwa Kada mbalimbali kwa kuwa utaratibu wa kuajiri na kupandishwa vyeo ndani ya Utumishi umekuwa ukibadilika kulingana na majukumu ya kiutendaji na maendeleo ya kiuchumi.

WIZARA YA NISHATI:

41. MHESHIMIWA KUNTI YUSSUF MAJALA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itasambaza umeme katika Kata za Handa, Lalta, Sanzawa na Mpendo.

42. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza transfoma ya 100 MVA katika *substation* ya Mbagala ili kuondoa tatizo la kukatika umeme katika Jimbo la Mbagala.

WIZARA YA KILIMO:

43. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya muda mrefu ya Mhe. Rais ya ujenzi wa Bwawa la umwagiliaji kwenye Bonde la Mto Mkomazi.

WIZARA YA MAJI:

**44. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA
(NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ya ujenzi wa bwawa la maji katika Kata ya Mikangaule Wilayani Nanyumbu itatekelezwa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**45. MHESHIMIWA BRYCESON MAGESSA
TUMAINI (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya Zimamoto katika Mji Mdogo wa Katoro ili kupunguza hatari ya moto iwapo utatokea ikizingatiwa kwamba kuna ongezeko kubwa la Wafanyabiashara katika Mji huo.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

46. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuanzisha Viwanda vya dawa na vifaa tiba hapa nchini ili kuacha kuagiza vifaa hivyo nje ya nchi.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

47. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha gharama za kuhamisha umiliki wa ardhi ambazo si rafiki hasa kwa wanyonge na kusababisha wengi kuwa na miliki bubu.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

48. MHESHIMIWA ALI HASSAN OMAR KING (JANG'OMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, wizi unapotokea kwenye akaunti ya benki ya mteja uliofanywa na mtumishi wa benki ni nani mwenye wajibu wa kumlipa mteja.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa lijadili na kuidhinisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2021/22 – 2025/26.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
09 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**